



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MSAJILI WA HAZINA**

TANGAZO LA SHINDANO LA UBUNIFU WA NEMBO

Ofisi ya Msajili wa Hazina inapenda kuwaalika wabunifu wa nembo katika shindano la kubuni nembo rasmi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina (OMH) ambayo itazingatia dira, dhima na majukumu ya Ofisi.

Sifa za nembo

1. Nembo inatakiwa iwe rahisi kutambulika na kusomeka iwapo itatumika katika maeneo tofauti kama vile vyombo vya usafiri, mabango, majengo, tovuti, mavazi, mikoba, "Business Card", matangazo ya televisheni na mitandao ya kijamii, pamoja na machapisho mengine.
2. Nembo iwe na rangi inayovutia na kuleta maana kwa kuzingatia dira, dhima na majukumu ya Ofisi, na kuambatanisha namba za rangi zinazotambuliwa na kompyuta "color code" (RGB/CMYK).

Vigezo vitakavyotumika katika kumchagua mshindi

- a. Urahisi wa Kutambulika: Nembo inapaswa kuwa wazi na inayoweza kutambulika kwa urahisi kwa matumizi mbali mbali kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 2.
- b. Maelezo ya maandishi na maana yake: Ubunifu huu unapaswa kuambatana na maelezo ya maandishi na maana ya kila alama iliyopo kwenye nembo.
- c. Uhalisia wa Ubunifu: Ubunifu utakaowasilishwa ni lazima uwe halisi na uwe umebuniwa na aliyetuma ubunifu huo na usiwe wa kunakili ubunifu wowote kutoka ndani au nje ya nchi.
- d. Lugha: Maneno yote au alama yoyote itakayotumika inapaswa kuwasilishwa na tafsiri yake katika lugha ya Kishwahili na Kiingereza.

Angalizo

- a. Ofisi ya Msajili wa Hazina itakuwa na haki ya kuisajili nembo itakayochaguliwa kama alama yake ya huduma.
- b. Nembo inapaswa kuwasilishwa katika "format" ya PDF, PNG, na JPEG
- c. Uamuzi wa Jaji wa shindano hili ndio utakuwa uamuzi wa mwisho

Zawadi:

Mshindi wa shindano hilo atazawadiwa fedha taslimu baada ya Menejimenti kuridhia na muhusika kuidhinisha juu ya matumizi ya Nembo.

Mawasiliano

Kila Mbunifu atapaswa kutuma nembo yake pamoja na barua ya kuwasilisha nembo hiyo kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ikionesha: Jina kamili, picha ya ukubwa wa passpoti ya muhusika, namba ya simu pamoja na anuani ya makazi. Nembo hiyo itumwe kupitia barua pepe ya alex.malanga@tro.go.tz kabla ya saa 11:00 jioni ya tarehe 28/02/2025.

Tangazo hili linapatikana pia katika tovuti (www.tro.go.tz) na akaunti ya Instagram ([ofisi_ya_msajili_wa_hazina](#)) ya Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Nehemiah Mchechu
MSAJILI WA HAZINA